



# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



## JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

**Na:5. Msimu wa Kilimo 2019/20 Tathmini Novemba 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Novemba 21-30, 2019**

### Muhtasari


- Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, wakulima wanaendelea na shughuli za palizi.
- Msimu wa mvua umeanza kwa maeneo ya Kigoma, Rukwa na Tabora na wakulima wameanza kupanda mazao.
- Kutokana na hali ya ukavu wa muda mrefu kwa maeneo mengi ya Shinyanga, Dodoma, Singida, Longido na Kiteto, wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2019

**K**atika kipindi hiki cha dikadi, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha kusogea kwa ukanda wa mvua katika eneo la ukanda wa kusini. Hata hivyo, uwepo wa mgandamizo mdogo wa hewa kusini magharibi mwa Madagascar kulisababisha kutoimarika kwa ukanda wa mvua wa Kitropikali katika maeneo mengi ya nchi. Hali hii ilisababisha mchango mdogo wa mvua katika maeneo mengi nchini. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

### MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2019

**K**atika dikadi hii vipindi vya mvua za wastani viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, kaskazini mashariki na magharibi mwa nchi na pwani ya kaskazini. Aidha mvua nyepesi iliripotiwa katika maeneo ya , nyanda za juu kusini mashariki pamoja ,nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kati. Kiasi cha mvua kilichoripotiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi ni kuanzia milimita 26 na hadi milimita 250 kama inavyoonesha katika ramani.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Novemba 11- 20, 2019

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2019

**H**ali ya unyevu wa udongo ilendelea kuimarika katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, wakulima waliopanda mapema wameendelea na palizi hususan katika maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini na ukanda wa pwani ya kaskazini isipokuwa mkoa wa Shinyanga ambapo msimu wa vuli umechelewa kuanza. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka ikiwamo mkoa wa Tabora, Rukwa na Kigoma msimu wa mvua umeanza na upandaji wa mazao uliendelea. Maeneo yaliyosalia wakulima wanaendelea na maandalizi ya mashamba kwa

ajili ya msimu unaotarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya Novemba hadi Disemba 2019. Katika kipindi cha siku kumi hizo, upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua za *Vuli* zinazoendelea kunyesha, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Dodoma, Singida, Longido na Kiteto ambako hali ya maji na malisho bado si ya kuridhisha.

### HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2019

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito vimeanza kuongezeka hususan maeneo yanayopata misimu miwili wa mvua kutokana na mvua za vuli zinazoendelea .

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha kusogea kwa ukanda wa mvua katika eneo la ukanda wa kusini. Vilevile, kuimarika kwa wimbi anga “Madden Julian Oscillation” katika kipindi hiki kunatarajiwa kusababisha kuimarika kwa mfumo wa utengenezaji mvua katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, magharibi, nyanda za juu kusini magharibi na kati mwa nchi. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

### HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA 21-30, 2019

**M**aeneo ya Kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na

Singida) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) kunatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) kunatarajiwa kupata hali ya ukavu kwa ujumla.

### HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019.

**M**vua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kwa shughuli za kilimo. Kwa maeneo ambayo mvua za msimu hazijaanza kunyesha wakulima wanashauriwa kuendelea kuandaa mashamba. Wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki. Pia wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.

### HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019.

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa mito kinatarajiwa kuongezeka katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la Ziwa Viktoria, Pangani na Wami/Ruvu. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania  
Horofa ya 3 - Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania